TANGAZO LA SERIKALI Na.1016 la tarehe 6/12/2024

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI), (SURA YA 288)

HATI

(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 58 (1))

HATI YA UANZISHAJI WA BODI YA HUDUMA NA UENDESHAJI WA SOKO LA SAMAKI LA KIMATAIFA LA FERI MAGOGONI YA MWAKA 2024

Jina

1. Hati hii itajulikana kama Hati ya Uanzishaji wa Bodi ya Huduma na Uendeshaji wa Soko la Samaki la Kimataifa la Feri Magogoni ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Hati hii itatumika katika Soko la Samaki la Kimataifa la Feri Magogoni.

Tafsiri

3. Katika Hati hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Huduma na Uendeshaji wa Soko la Samaki la Kimataifa la Feri Magogoni iliyoanzishwa chini ya kanuni ya 4 ya Hati hii;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam;

"Kamati ya wadau wa soko" maana yake ni Kamati ya wadau wa soko iliyoundwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo ya Uendeshaji wa Soko la

Samaki la Kimataifa la Feri Magogoni ya Mwaka 2024;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mkuu wa soko" maana yake ni mtumishi wa umma kutoka Halmashauri atakayeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia shughuli za kila siku za soko;

"soko" maana yake ni Soko la Samaki la Kimataifa la Feri Magogoni lililopo ndani ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam;

"wadau wa soko" maana yake ni wafanyabiashara binafsi, taasisi, kampuni au kikundi cha watu wanaofanya biashara au shughuli zao katika soko na kusajiliwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo ya Uendeshaji wa Soko la Samaki la Kimataifa la Feri Magogoni ya Mwaka 2024; na

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya serikali za mitaa.

Kuanzishwa kwa Bodi

4.-(1) Kutakuwa na Bodi ya Huduma na Uendeshaji wa Soko la Samaki la Kimataifa la Feri Magogoni ambayo katika Hati hii itajulikana kama Bodi.

(2) Bodi inaanzishwa kwa madhumuni yafuatayo-

(a) kuimarisha huduma za uendeshaji wa soko;

(b) kuweka mipango endelevu ya kuimarisha huduma za soko;

(c) kusaidia uendelezaji wa miundombinu ya soko;

(d) kutafuta vyanzo vya mapato kutoka kwa wahisani kwa lengo la kuinua ufanisi wa utoaji wa huduma za soko; na

(e) kubuni na kuanzisha vyanzo vipya vya mapato ya soko.

(3) Makao makuu ya Bodi yatakuwa katika eneo la soko.

Majukumu ya Bodi

5. Katika kuhakikisha kuwa inatimiza madhumuni ya kuanzishwa kwake, Bodi itakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kusimamia masuala na shughuli zote zinazohusu soko na usimamizi wa Sheria Ndogo zinazohusu soko;

(b) kuratibu na kusimamia shughuli za maendeleo ya soko;

(c) kubuni mbinu na mipango itakayoweza kuimarisha huduma za soko;

(d) kupitisha bajeti ya uendeshaji wa soko na kuiwasilisha Halmashauri;

(e) kutoa taarifa ya utekelezaji wa malengo na mipango ya soko kwa uongozi na Wadau wa soko;

(f) kuishauri Halmashauri namna ya kuimarisha ubora wa huduma zinazotolewa katika soko;

(g) kupokea na kujadili taarifa za robo mwaka za mapato na matumizi ya soko;

(h) kuhakikisha fedha za kuendesha shughuli za soko zilizotengwa kwenye bajeti zinatumika kama ilivyokusudiwa;

(i) kutekeleza mapendekezo ya Kamati ya wadau wa soko na Kamati za Bodi;

(j) kupokea na kusimamia utekelezaji wa miongozo, kanuni na taratibu mbalimbali kutoka Halmashauri;

(k) kuwasilisha taarifa za mapato na matumizi kwa Halmashauri kila robo ya mwaka wa fedha;

(l) kusimamia ulinzi, usalama na usafi wa soko; na

(m) kufanya shughuli nyingine zilizoidhinishwa kwa mujibu wa Hati hii.

Wajumbe wa Bodi

6.-(1) Bodi itakuwa wajumbe tisa kama ifuatavyo:

(a) Mwenyekiti ambaye atapatikana kwa utaratibu wa kutangaza kwa umma nafasi ya Mwenyekiti wa Bodi na atakuwa na sifa zifuatazo:

(i) awe ni raia wa Tanzania na mkazi wa Dar es salaam;

(ii) awe na umri usiopungua miaka ishirini na moja na usiozidi miaka sitini na mitano;

(iii) awe na shahada ya kwanza katika fani yoyote;

(iv) awe na uzoefu na uwezo wa kuongoza katika shughuli za huduma ya jamii;

(v) awe na akili timamu;

(vi) asiwe amewahi kutiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai;

(vii) asiwe na wadhifa wa kisiasa au uongozi wa ngazi yoyote katika chama cha siasa; na

(viii) asiwe mtumishi wa umma;

(b) Wajumbe wanne kutoka Kamati ya wadau wa soko kama ifuatavyo:

(i) Mwenyekiti wa Kamati ya wadau wa soko;

(ii) wajumbe wawili kutoka katika Kamati ya wadau wa soko ambao angalau mmoja kati yao lazima awe mwanamke na watachaguliwa na Kamati ya wadau wa soko; na

(iii)Mwakilishi mmoja kutoka umoja wa wavuvi wadogo ambaye atachaguliwana Kamati ya wadau wa soko.

(c) Wajumbe wanne wanaoingia katika Bodi kwa nyadhifa zao kama ifuatavyo:

(i)Mjumbe mmoja atakayeteuliwa na Mkurugenzi kutoka miongoni mwa watumishi wa umma mwenye utaalam katika fani ya uvuvi;

(ii)Mwakilishi mmoja wa Wizara yenye dhamana ya masuala ya uvuvi ambaye hajafikia wadhifa wa Mkurugenzi;

(iii)Mkuu wa Kitengo kinachohusika na uvuvi katika Halmashauri; na

(iv)Mwakilishi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya isipokuwa Mkuu wa Wilaya au Katibu Tawala wa Wilaya.

Uthibitisho wa wajumbe

7.-(1) Wajumbe wa Bodi watathibitishwa na Waziri kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yao.

(2) Katika kutekeleza masharti ya aya ndogo ya (1), Waziri anaweza kukataa kuthibitisha jina la mjumbe yeyote na kuelekeza taasisi inayowasilisha jina la mjumbe huyo kuwasilisha jina la mtu mwingine.

(3) Baada ya wajumbe wa Bodi kuthibitishwa na Waziri, Mkurugenzi atawasilisha majina yao katika Baraza la Madiwani kwa taarifa.

(4) Mara baada ya majina ya Wajumbe wa Bodi kuthibitishwa na Waziri, wajumbe wa Bodi wataapa kiapo cha uaminifu na uadilifu kama kilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Hati hii.

Katibu wa Bodi

8.-(1) Mkuu wa soko atakuwa Katibu wa Bodi na kwa nafasi hiyo atakuwa ndiye mtendaji mkuu wa Bodi.

(2) Katibu wa Bodi atakuwa na majukumu yafuatayo-

(a) kuandaa vikao vya Bodi;

(b) kuandika muhtasari wa vikao vya Bodi;

(c) kutunza kumbukumbu zote za vikao vya Bodi;

(d) kusambaza barua za wito wa vikao vya Bodi kwa wajumbe;

(e) kuwasilisha taarifa za utendaji wa Bodi kwa Halmashauri kila baada ya miezi mitatu;

(f) kuandika kumbukumbu za mikutano na kuzihifadhi;

(g) kusimamia na kufuatilia maamuzi ya vikao vya Bodi; na

(h) kusimamia mienendo ya watumishi, taratibu na utekelezaji wa maagizo ya Bodi.

(3) Katibu wa Bodi hatakuwa na haki ya kupiga kura katika vikao vya Bodi.

Muda wa kuwa madarakani

9.-(1) Mjumbe wa Bodi atashika nafasi kwa muda wa miaka mitatu tangu tarehe ya kuteuliwa

kwake na anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja.

(2) Bila kuathiri masharti ya aya ndogo ya (1), mjumbe atapoteza nafasi yake endapo kutatokea mojawapo ya mambo yafuatayo:

(a)kufariki dunia;

(b) kuwa na maradhi ya mwili au akili yanayoathiri utendaji wake wa kazi;

(c) kufanya ubadhilifu wa fedha na mali za soko;

(d) kutokuhudhuria vikao vitatu mfululizo bila taarifa;

(e) kukiuka masharti ya Hati hii au Sheria Ndogo ya Uendeshaji wa Soko la Samaki la Feri Magogoni ya Mwaka 2024;

(f)kuhamasisha migogoro au uvunjifu wa amani sokoni;

(g) kutolipa kodi, ushuru, ada na mapato ya Serikali kwa kipindi cha miezi mitatu mfululizo;

(h) kutoa siri za vikao vya Bodi bila ya idhini ya Bodi; au

(i) kupoteza mojawapo ya sifa zilizomfanya kuwa Mjumbe wa Bodi.

Utaratibu wa kufuatwa kabla ya kumuondoa mjumbe wa Bodi

10. Taratibu zifuatazo zitatumika endapo mjumbe wa Bodi atatuhumiwa kwa kosa lolote litakalosababisha kupoteza sifa ya kuwa mjumbe wa Bodi:

(a) taarifa ya mjumbe atakayetuhumiwa itawasilishwa katika kikao cha dharura cha Bodi ili iweze kujadiliwa;

(b) Katibu wa Bodi atamjulisha mjumbe kwa maandishi tuhuma zinazomkabili na mtuhumiwa

atapewa siku kumi na nne za kujibu tuhuma hizo kwa maandishi;

(c) mara baada ya siku kumi na nne kuisha Katibu ataitisha kikao cha dharura cha Bodi na kujadili tuhuma zinazomkabili mjumbe wa Bodi na Bodi itatoa mapendekezo na kuwasilisha kwa Mkurugenzi;

(d) mara baada ya kupokea mapendekezo ya Bodi Mkurugenzi atawasilisha kwenye mamlaka husika kwa ajili ya uamuzi.

Utaratibu wa kujaza nafasi ya iliyo wazi

11.-(1) Endapo nafasi ya mjumbe itakuwa wazi, nafasi hiyo itajazwa kwa utaratibu uliotumika kumpata mjumbe kwa kuteuliwa kushika nafasi hiyo kwa kipindi kilichobaki na anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine.

(2) Bila kuathiri masharti ya aya ndogo ya (1), hakuna uteuzi utakaofanyika wa kujaza nafasi ya mjumbe ikiwa muda uliosalia kabla ya Bodi kumaliza muda wake ni miezi sita au pungufu ya miezi sita.

Uwajibikaji wa Bodi

12. Katika kutekeleza majukumu yake, Bodi itawajibika kwa Halmashauri na itapokea maelekezo na miongozo itakayotolewa na Halmashauri.

Kuvunjwa kwa Bodi

13.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Hati hii, Halmashauri itakuwa na mamlaka ya-

(a) kuionya Bodi kwa maandishi; au

(b) kuivunja Bodi, baada ya kushauriana na Waziri, endapo-

(i) baada ya kutoa onyo la maandishi mara mbili utendaji wa Bodi utaendelea kutoridhisha; au

(ii) theluthi mbili ya wajumbe watapoteza sifa ya kuwa wajumbe wa Bodi.

(2) Endapo Bodi itavunjwa, wajumbe wote wa Bodi watapoteza nafasi zao na hawatakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa wajumbe wa Bodi kwa muda wa miaka sita tangu tarehe ya kuvunjwa kwa Bodi.

(3) Endapo Bodi itavunjwa Mkurugenzi atateua Kamati maalumu yenye wajumbe saba kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Bodi kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja.

Kikao cha Bodi

14.-(1) Bodi itafanya kikao chake cha kawaida kila baada ya miezi mitatu.

(2) Kikao cha Bodi kitaendeshwa na Mwenyekiti na endapo Mwenyekiti atashindwa kuendesha kikao hicho kwa sababu yoyote ile wajumbe waliohudhuria kikao husika watamchagua mjumbe kutoka miongoni mwao kuendesha kikao hicho.

(3) Akidi katika kikao cha Bodi itakuwa ni nusu ya wajumbe wote wa Bodi.

(4) Taarifa ya kikao cha Bodi itatolewa na Katibu wa Bodi si chini ya siku saba kabla ya tarehe ya kikao.

(5) Bila kujali aya ndogo ya (4), wajumbe wa Bodi wanaweza kuridhia kuendelea na kikao ambacho taarifa yake imetolewa chini ya muda wa siku saba.

(6) Mwenyekiti wa Bodi anaweza kuitisha kikao cha dharura baada ya kujadiliana na Mkuu wa Soko au Mkurugenzi akieleza sababu ya kikao hicho kuitishwa.

(7) Taarifa ya kikao cha dharura cha Bodi itatolewa ndani ya siku tatu baada ya makubaliano ya Mwenyekiti wa Bodi na Mkurugenzi.

(8) Bila kuathiri masharti ya aya ndogo ya (6), hakutakuwa na kikao cha dharura zaidi ya kimoja kitakachoitishwa ndani ya miezi mitatu.

Uamuzi wa Bodi

15.-(1) Uamuzi wa Bodi utakuwa ule ulioungwa mkono na zaidi ya nusu ya wajumbe wote wa Bodi waliohudhuria kikao husika.

(2) Kila Mjumbe wa Bodi atakuwa na kura moja na endapo itatokea idadi ya kura kulingana, Mwenyekiti wa Bodi au mjumbe anayeendesha kikao atakuwa na kura ya ziada.

Kutunza siri za ajadiliano ya vikao vya Bodi

16. Mjumbe wa Bodi hatoruhusiwa kutoa taarifa ya suala lolote lililojadiliwa katika vikao vya Bodi au Kamati za Bodi bila ya ruhusa ya Bodi.

Kusainiwa kwa hati au Maagizo ya Bodi

17. Maagizo, maelekezo, taarifa au nyaraka yoyote itakayotolewa na Bodi au kwa niaba ya Bodi itatiwa saini na Mwenyekiti au Katibu wa Bodi.

Uthibitishaji wa Mihutasari ya vikao

18. Muhtasari wa kikao cha Bodi utathibitishwa katika kikao kinachofuata na utasainiwa na Mwenyekiti wa kikao na Katibu wa Bodi.

Bodi kualika Watu wengine

19. Bodi inaweza kumwalika mtu yeyote kwenye vikao vyake kama kutakuwa na haja ya kufanya hivyo lakini mtu huyo hatakuwa na haki ya kupiga kura.

Kamati ya Bodi

20. Bodi inaweza kuunda Kamati kutoka miongoni mwa wajumbe wake kwa madhumuni ya kushughulikia masuala mahsusi ya soko na Kamati itakayoundwa itawasilisha taarifa zake kwenye Bodi.

Mikutano na wadau

21.-(1) Kutakuwa na kikao cha Bodi pamoja na Kamati ya wadau wa soko kitakachofanyika kila baada ya miezi sita.

(2) Bila kuathiri masharti ya aya ndogo ya (1), katika kutekeleza majukumu yake, Bodi inaweza kukutana na wawakilishi wa wafanyabiashara wote na viongozi wa soko wakati wowote itakapohitajika.

Aina ya posho

22.-(1) Wajumbe wa Bodi watalipwa posho mbalimbali kwa viwango vitakavyopendekezwa na Halmashauri.

(2) Posho itakayolipwa kwa wajumbe wa Bodi itakuwa kama ifuatavyo-

(a) posho ya kuhudhuria kikao;

(b) posho ya wajumbe wa Bodi kwa mwaka;

(c) posho ya safari; na

(d) posho ya madaraka kwa Mwenyekiti na Katibu

Mipango

23.-(1) Katibu wa soko ataandaa mpango wa bajeti ya soko na kuiwasilisha katika Bodi kwa kuzingatia ratiba ya maandalizi ya bajeti ya Halmashauri.

(2) Bodi itapokea, itajadili, itachambua na kuidhinisha mpango wa bajeti na kuwasilisha kwa Halmashauri kwa ajili ya kuidhinishwa kupitia Kamati za Halmashauri.

(3) Bodi inaweza kufanya mapitio ya bajeti ya nyongeza kama kutakuwa na haja ya kufanya hivyo na kama mazingira yataruhusu.

Vyanzo vya mapato

24.-Vyanzo vya mapato ya soko ni-

(a)fedha zote zitakazopokelewa kutokana na ada, ushuru na kodi zitakazotolewa na Wadau wa soko;

(b)fedha zitakazotolewa na wahisani wa ndani na nje ya Halmashauri;

(c) michango ya watu binafsi wanaoishi ndani na nje ya Halmashauri; na

(d)fedha zozote halali ambazo soko inaweza kupata kutoka mahali pengine popote.

Akaunti ya mapato

25.-(1) Halmashauri itafungua akaunti maalumu ambayo itatumika kuhifadhi mapato yote ya soko.

(2) Akaunti ya mapato itakuwa chini ya usimamizi wa Mkurugenzi na fedha za matumizi ya soko zitahamishwa kutoka katika akaunti hiyo na kuingizwa katika akaunti ya matumizi ya soko.

(3) Bila kuathiri masharti ya aya ndogo ya (2), fedha zitakazotolewa kwa ajili ya matumizi ya soko zitakuwa ni asilimia sabini ya mapato na asilimia thelathini itarejeshwa Halmashauri.

Akaunti ya matumizi

26.-(1) Kutakuwa na Akaunti moja ya soko ambayo itakuwa ni akaunti ya matumizi na itatumika kwa matumizi yote yatakayofanywa na soko.

(2) Watia saini kwenye akaunti ya soko watakuwa kama ifuatavyo:

(a) Mkuu wa soko au Mweka Hazina wa Halmashauri kwa upande mmoja; na

(b) Mhasibu wa soko au Afisa mwingine yeyote wa Halmashauri aliyeko sokoni atakayeidhinishwa na Bodi kwa upande mwingine.

(3) Akaunti ya matumizi ya soko itakaguliwa kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za usimamizi wa fedha za umma.

Matumizi ya fedha za soko

27. Fedha zitakazoingizwa katika akaunti ya matumizi ya soko zitatumika kwa madhumuni yafuatayo:

(a) masuala yanayohusiana na uendeshaji na uimarishaji wa soko;

(b) kutekeleza matumizi yote yaliyo katika bajeti kulingana na vipaumbele vya soko na mpango wa matumizi ya fedha zilizoidhinishwa; na

(c) Kutekeleza suala au shughuli yoyote muhimu itakayoonekana inafaa na itakayoidhinishwa na Bodi.

Taratibu za ununuzi

28. Katika kufanya ununuzi, Bodi itatakiwa kuzingatia taratibu za ununuzi wa umma zilizoainishwa katika Sheria ya Ununuzi wa Umma.

Taarifa ya matumizi

29. Bodi itakuwa na wajibu wa kuandaa taarifa ya matumizi ya fedha katika akaunti ya matumizi na kuiwasilisha kwa Halmashauri kila mwezi.

Kufutwa kwa Hati T S Na. 609 la 2019

30. Hati Rasmi (Uanzishaji wa Bodi ya Huduma ya Soko la Samaki Feri) ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilala ya Mwaka 2019 imefutwa.

JEDWALI

(Limetengenezwa chini ya aya ya 7(4))

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

KIAPO CHA MJUMBE WA BODI

Mimi ……………………………………………..…..... naapa au natamka kwa dhati kwamba nitaitumikia Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa wadhifa wangu wa Ujumbe wa Bodi ya Huduma na Uendeshaji wa Soko la Samaki la Kimataifa la Feri Magogoni na kwamba nitahifadhi, nitalinda na kutetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sheria za Tanzania na Sheria Ndogo za Jiji la Dar es Salaam kama zilivyowekwa kwa mujibu wa Sheria na kwamba nitaitumikia Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa uaminifu, kwa uwezo na moyo wangu wote.

(Ewe Mwenyezi Mungu nisaidie)

Kiapo au Tamko hili limetolewa hapa:………………………………………
Na……………………………………………………………
Leo tarehe……………Mwezi wa…………….Mwaka 20……….

Mbele ya:………………………………………..
Jina:………………………………………………
Cheo:…………………………………………….
Saini:……………………………………………
Anuani…………………………………………..

Lakiri ya Jiji la Dar es Salaam imegongwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa katika Mkutao wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam uliofanyika tarehe 6/3/2023 na kushuhudiwa Lakiri hiyo ikigongwa mbele ya:-

JOMAARY MRISHO SATURA,
Mkurugenzi wa Jiji,
Halmashauri ya jiji,
Dar es salaam

MHE. OMARY KUMBILAMOTO,
Msahiki meya,
Halmashauri ya jiji,
Dar es salaam

L.S

NAKUBALI,

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
Waziri wa Nchi OR-Tamisemi

Dodoma,
29 Agosti, 2024